



## TAARIFA KWA UMMA

### MABADILIKO YA ADA ZA HUDUMA YA NDOA NA TALAKA

Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhadini (RITA) unapenda kuwatangazia wananchi kupanda kwa Ada za Huduma katika Kitengo cha Ndoa na Talaka kama ilivyotangazwa katika katika Gazeti la Serikali Na.223 la tarehe 12/6/2015.

Ada mpya zimeanza kutumika kuanzia Tarehe 01 Disemba 2015 na ni kama ifuatavyo;

Na	AINA YA HUDUMA	ADA (TShs.)
1	Cheti cha Ndoa cha Msajili Mkuu wa Ndoa	20,000
2	Cheti cha Ndoa ambayo haijawahi kuandikishwa	20,000
3	Cheti cha Ndoa iliyofungwa Nje ya Nchi	100,000
4	Cheti cha Talaka	20,000
5	Cheti cha Talaka iliyotolewa Nje ya Nchi	100,000
6	Leseni ya kufunga Ndoa mahali maalum	200,000
7	Shahada ya kutokuwepo pingamizi	200,000
8	Barua ya kutokuoa/ kutokuolewa	100,000
9	Uthibitisho wa cheti cha Ndoa/Talaka	20,000
10	Ada ya upekuzi katika daftari la Ndoa/Talaka	30,000
11	Kuandikisha uthibitisho wa ndoa iliyobadilishwa kuwa ya mke mmoja au ya wake wengi	30,000
12	Marekebisho katika cheti cha Ndoa na Talaka	60,000
13	Leseni ya kufungisha Ndoa	30,000
14	Ndoa ya haraka	100,000
15	Ada ya ruhusa ya kufungisha Ndoa mahali maalum kwa mgonjwa	20,000
16	Ndoa ya serikali ya kutangaza siku 21	50,000
17	Shahada za Ndoa zinazotolewa kwa wasajili wa wilaya na viongozi wa dini:-	
	Shahada 5	50,000
	Shahada 10	100,000
	Shahada 20	200,000
	Shahada 50	500,000

RITA inapenda kuwakumbusha wananchi wote kwamba malipo yote kwa Huduma tajwa hapo juu na nyingine zote zinazotolewa na Wakala yafanyike kupitia: **Benki ya NMB** Akaunti namba 20601100078 au **M Pesa** na **Tigo Pesa** kwa Namba ya kampuni 240099. Baada ya Malipo hakikisha unapata, katika Ofisi za RITA, risiti ya Serikali inayolingana na Fedha ulizolipa. Tunasisitiza kwamba Ofisi za RITA kote nchini hazipokei fedha taslimu kwa ajili ya Malipo ya Ada ya huduma yoyote.

Kwa maelezo zaidi, fika katika Ofisi za RITA zilizo katika Ofisi za Wakuu wa Wilaya kote nchini au piga simu namba 0719 017 217.

**“ RITA kwa Maisha yako ”**

Imetolewa na:

**Kitengo cha Masoko na Mawasiliano**

**RITA.**